**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KAMA YALIVYOWASILISHWA NA MHE. PAULINE GEKUL (MB.) MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA. KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Mei, 2016.

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwa kunipa uhai na afya ya kusimama hapa mbele ya Bunge lako tukufu siku ya leo.

**Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii kuishukuru familia yangu, ndugu,jamaa na marafiki husani wananchi wangu ambao wamekuwa na mimi bega kwa bega katika harakati za maendeleo ,japo hawanioni tena live katika runinga zao kwa sababu ya fitina za kisiasa zinazofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo kwa sasa imepewa jina maarufu kama "Serikali ya Magufuli" za kufifisha demokrasia, kuondoa uhuru wa habari nchini na kuupumbaza umma kwa siasa nyepesi ambazo muda sio mrefu umaarufu wake utakuwa umekwisha kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Nina waahidi sitachoka kuwapigania hata kama hawanioni wala kunisikia kwenye vyombo vya habari jinsi ninavyowapigania humu ndani ya bunge. Mimi pamoja na wenzangu wa Kambi ya Upinzani tutaendeea kuikosoa serikali ili ifanye wajibu wake na ninyi muweze kuyajua madudu mengi yanayofichwa na serikali,kuamsha ari ya kufuatilia habari, kujifunza na kupambanua wajibu wa serikali kwenu kama tulivyofanya huko awali .

**Mheshimiwa Spika,** kwa upekee zaidi napenda kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni,Mh .Freeman Aikael Mbowe Mbunge wa Hai kwa kuniamini na kuniteuwa kuwa Waziri Kivuli katika Wizara hii.Napenda kumuhakikishia kamanda wake niko imara na nitapiga jaramba mpaka kieleweke.

## 2.0 UTENDAJI WA SERIKALI YA AWAMU YA TANO .

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuifahamisha serikali hii ya awamu ya tano kuwa ***"your enemy is not the person who opposes you. It is the person who congratulates you when doing crap."***Adui yako si yule unaye tofautiana nae . Adui ni yule anayekupongeza pale unapofanya ujinga. Ni vyema zaidi serikali chini ya Rais wa Tano wa Tanzania wakaitafakari kwa kina kauli hii.

**Mheshimiwa Spika**, kuna uzembe mkubwa ndani ya serikali hususani katika wizara hii inayoshughuika na mambo ya Mazingira na Muungano. Mambo mengi yanafanywa kiholela bila kufuata taratibu na kuheshimu sheria, sera na miongozi mbalimbali ambayo tulijiwekea wenyewe na tukairidhia. Inaudhi kuona hakuna hatua stahiki zinazochukuliwa badala yake wananchi wanazidi kuumia kwa hali ngumu ya kimaisha.

**Mheshimiwa Spika,** mazingira ni neno lenye dhana pana sana, kila sekta ina muktadha wake kuhusiana na mazingira, kutokana na muktadha ya Serikali iliyopo sasa imeona mazingira ni taka ngumu au za maji zinazotoka viwandani na ndio maana Kamati inayoshughulikia mazingira ni ile ya viwanda na Biashara.

**Mheshimiwa Spika,** mazingira ni zaidi ya kufikiria taka ngumu au maji ya taka, mazingira ni uhai wetu kwa vizazi vya leo na vijavyo, hii inaendana na kanuni ambayo inasema "***today's world is not ours but we borrow that from the future generation, so we have to use it sustainably".*** Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba Dunia tuliyonayo sasa sio yetu bali tumeiazima kutoka kizazi kijacho, hivyo tunatakiwa tuitumie kwa uendelevu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sekta ya kilimo mazingira ni aina yoyote ya kilimo itakayopelekea mazao kushindwa kustawi vyema katika eneo la ardhi husika kutokana na udongo kuwa sumu au kuisha rutuba yake. Kwa upande wa misitu, uharibifu wa mazingira kwao ni ukataji/ufyekaji wa miti **(deforestation)** bila ya kupanda miti mipya **(afforestation**), kwa upande wa uzalishaji viwanda mazingira kwa muktadha wao unajikita sana kwenye aina ya mitambo inayotumika katika uzalishaji kama inauwezo wa ku-recycle taka zake na vile vile hewa ukaa inazalishwa kwa kiwango gani. Vivyo hivyo kwa sekta

ya madini uchimbaji madini usiofuata taratibu sahihi za utunzaji wa kemikali zinazotumika na pia kutokufukia mashimo ili kuirudisha ardhi katika uhalisia wake na kwa sekta ya masoko kutokuzoa taka zinazozalishwa sokoni na kuzipelekea katika maeneo yaliyotengwa nalo ni uchafuzi wa mazingira pia kwa upande wa baharini na maziwa mazingira yanaongelewa kwa muktadha wake tofauti na sekta tajwa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** Ni ukweli pia kuwa dhana ya mazingira ina tafsiri tofauti kwa jamii zinazoishi mijini na zile zinazoishi vijijini kwa kulingana na hali halisi inayowawezesha kumiliki na kuzitumia rasilimali zinazowazunguka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa jukumu la kutoa elimu kwa umma juu ya mazingira imekasimiwa kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira kwa niaba ya Serikali, litoe elimu ya mazingira kulingana na muktadha wa kisekta. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kwa njia hii migogoro iliyokuwepo kati ya Serikali na wananchi hasa wale waliokuwa wamejenga maeneo ambayo ambayo kwa mujibu wa Serikali ni hatarishi na hivyo walibomolewa nyumba zao.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo la kuwaelewesha wananchi ni lazima liende sambamba na kuzielewesha taasisi za umma ambazo zinatoa huduma kadhaa kwa wananchi. Kama Mamlaka za Maji na Shirika la Umeme zingekuwa na uelewa

mpana kuhusiana na dhana pana ya mazingira kwenye maeneo hayo hatarishi zisingepeleka huduma kwa wananchi na wananchi wasingejenga nyumba zao, Sambamba na hilo kama halmashauri maeneo husika zingekuwa na uelewa mpana zisingetoa leseni za makazi na pia zinalipisha wamiliki kodi za majengo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa kimsingi uzembe mkubwa ulifanywa na Serikali kwa kupitisha sheria na kushindwa kuifanya sheria hiyo ieleweke kwa wananchi na taasisi zake zote, Kambi Rasmi inaitaka Serikali kuchukua jukumu la kuhakikisha wahanga wote wanafidiwa kwa kadri wahanga walivyopoteza mali zao.

## 3.0 MAZINGIRA NA SHUGHULI ZA KIUCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** athari za kimazingira zinakuwa kubwa kutokana na kuongezeka kupita kiasi kwa shughuli za kiuchumi bila ya kuangalia hali halisi, uchimbaji wa madini, kilimo kinachotumia mitambo mikubwa na kuufanya udongo kuwa mwepesi kiasi cha kuondolewa na maji ya mvua pamoja na upepo, ufugaji mifugo mingi katika eneo dogo kutokana na eneo la malisho kuchukuliwa kwa ajili ya shughuli zingine za kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa lugha rahisi ni kuwa uendelevu na kukua kwa uchumi wetu kama nchi kunategemea ni kwa jinsi

gani kama nchi tumejipanga vizuri kuhakikisha mazingira kwa kila sekta inakuwa endelevu? Kambi Rasmi ya Upinzani inaelewa kuwa Mpango wa awamu ya pili wa miaka mitano, unalenga katika kuhakikisha nchi yetu inakuwa nchi ya kipato cha kati ambapo mchango mkubwa utokane na sekta ya viwanda. Mategemeo makubwa ya uwepo wa viwanda ni kutokana na kuwa na uwezo utakaokuwa endelevu wa uzalishaji wa malighafi.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kufikiria kuwa na uchumi wa viwanda ni lazima tutazame kuwekeza kikamilifu katika kuhakikisha kuwa mazingira yetu yanalindwa na tuwe na mipango mapema ya kuanza kufanya tathimini ya kimazingira kabla ya kutekeleza mradi wowote ule kwa ajili ya kuwa na uchumi endelevu unaolinda mazingira endelevu.

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wowote ambao tumepanga kuutekeleza kama utakuwa haukuzingatia ***aspect*** ya mazingira katika muktadha wa sekta husika ni dhahiri tumeshindwa kabla ya mpango wenyewe haujatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imetoa angalizo hilo kutokana na ukweli kwamba bajeti inayopangwa iwe katika sekta ya Kilimo, sekta ya mifugo, sekta misitu, sekta ya biashara na sekta zingine, ***Aspect*** ya mazingira ni muhimu sana ili kuifanya sekta husika kuwa endelevu na kwetu bado tuko nyuma. Hiyo ni dalili kwamba **sustainability** yetu katika

yale tunayoyapanga bado tuko nyuma hatua kadhaa ili tufanikiwe.

**Mheshimiwa Spika,** madhara ya shughuli za kiuchumi kwenye mazingira yanonekana wazi, ziwa Babati sasa hivi limejaa udongo unaotokana na shughuli za kiuchumi jambo ambalo linasababisha mafuriko ya mara kwa mara kwa wakazi wa maeneo ya jirani. Kujaa kwa bwawa la kuzalisha umeme la Mtera pindi mvua inaponyesha, japokuwa maji yanakuwa sio mengi ila ni kutokana na kujaa kwa udongo ***(siltation***) unaosombwa na maji ya mvua.

**Mheshimiwa Spika**, haya yote ni athari za kutokusimamia vyema sheria husika zinazosimamia shughuli za uzalishaji. Matatizo makubwa kwa mujibu taarifa ya wizara inaonesha kuwa uchache wa watumishi kwenye Baraza la Usimamizi wa Mazingira ni hoja ambayo imelifanya Baraza kushindwa kutimiza majukumu yake, vilevile ufinyu wa bajeti ambayo inatengwa na Bunge umepelekea Baraza kukosa fedha na badala yake linategemea kujiendesha kwa kutegemea ***fine*** na tozo ndizo zinatumika kuendesha baraza.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muendelezo huu wa kukosekana kwa au kupungua kwa fedha za matumizi mengineyo ni dhahiri viwanda vinavyotakiwa kujengwa katika awamu ya pili ya mpango wa maendeleo vinaweza kujengwa bila ya kufanyika kwa tathmini ya mazingira katika maeneo husika.

Hii ni hatari sana kwani hapo mbeleni kunaweza kuwepo na madhara makubwa katika mazingira yetu.

**Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni** , tunalishauri Bunge na Serikali kama kweli tunadhamiria kuwa na uchumi wa viwanda ni lazima tuongeze bajeti katika wizara hii na hasa kwa ajili ya shughuli za Baraza ili liweze kufanya tathimini ya mazingira kabla ujenzi na ufufuaji wa viwanda husika haujaanza kutekelezwa, ili uzalishaji utakapoanza pasiwepo na athari kubwa katika mazingira yetu.

## 4.0 MABADILIKO YA TABIA YA NCHI

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi, ambayo ni matokeo ya uharibifu mkubwa wa mazingira umeleta athari kubwa katika sekta mbalimbali za maendeleo ya jamii na sekta zingine ziko katika hatari ya kuathirika pia, sekta hizi ni nishati,kilimo na usalama wa chakula, maji, mifugo kwa kuzuka kwa magonjwa ya milipuko, uvuvi, misitu, wanyamapori, afya, miundombinu,utalii n.k

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ikiwa moja ya nchi zinazoendelea inahitaji wananchi wetu kujengewa uwezo wa kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi na hiyo kuwa ni kipaumbele cha kwanza. Upunguzaji wa uzalishaji na ongezeko la hewa ukaa iwe ni kipaumbele cha pili. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kwa kuzingatia mambo haya

mawili ni dhahiri madhara yanayojitokeza au yanayonyemelea sekta muhimu kwa uchumi wa nchi zitakuwa zimesalimika au madhara yatapungua kwa kiwango kikubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi hii ya Makamu wa Rais inatambua uzito wa tatizo la mabadiliko ya tabia ya nchi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa joto kali hadi kufikia nyuzi joto 36, sambamba na hayo kumekuwa na mvua kubwa zilizosababisha mafuriko katika maeneo mbalimbali nchini, kuyeyuka kwa theluji ya mlima Kilimanjaro, kupungua kwa vina vya maji katika mabwawa,mito, maziwa, na hata bahari,kubadiliko kwa majira ya mwaka n.k

**Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni,** inataka kujua serikali ina mipango gani endelevu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ikiwemo kuandaa sera mahususi na kuwa na sheria ya kusimamia utekelezaji wa sera husika.Aidha tunataka kujua tumejipanga vipi kutekeleza kwa vitendo mikataba yote ya kimataifa ambayo tumeiridhia inayohusiana na mabadiliko ya Tabia nchi.

## 4.1 MIRADI YENYE HARUFU YA UFISADI :

### 4.1.1 mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya jiji la dar es salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu lengo lake kuu lilikua ni **kujenga ukuta wa kuzuia bahari isiharibu 'Ocean Road' na Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere Kigamboni.** Mwezi Desemba mwaka 2011 Bodi ya Mfuko wa Dunia wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi "Adaptation Fund Board-AFB" wenye makao makuu huko Bonn, Ujerumani ilipitisha mradi huu wa kuisaidia Tanzania wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni tano (USD 5 million). Mradi ulikuwa ukitekelezwa kupitia UNEP kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwezi, Mei 2012 hadi Aprili 2017.Ulitakiwa kusimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikisha jiji la Dar Es Salaam na halmashauri zake.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi ulikuwa ufanye mambo yafuatayo;

a) Kutenegeneza baadhi ya miundombinu ya majitaka ya jiji la Dar es salaam zilitolewa Dola za Kimarekani 200,000
b) Kukarabati na kuimarisha ukuta wa Bahari (urefu usiopungua 1.335 km) ulioharibika katika maeneo ya Ocean Road na Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere zilitolewa Dola za Kimarekani 3,337,500
**c)** Uhifadhi wa mikoko (40ha) ya mwambao wa jiji la Dar es salaam ili kupunguza kasi ya uharibifu wa fukwe; Dola za Kimarekani 35,000

d) Kulinda matumbawe (2,000 $m^2$) maeneo ya Dar es Salaam ambako yameharibiwa ; Dola za Kimarekani 110,000

e) Kutengeneza maeneo ya ukanda wa Bahari "Shoreline stabilization" (1500m x 20m); Dola za Kimarekani 67,500

f) Kukuza uelewa wa mabadiliko ya tabianchi na kuuhisha "integration" suala la mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya kuhifadhi maeneo ya fukwe za Dar Es Salaam. Dola za Kimarekani 235,000;

g) Kutengeneza Mpango Kazi wa utunzaji wa mazingira ya pwani kuhimili mabadiliko ya tabinachi "Ecosystem Based Integrated Coastal Area Management Action Plan": Dola za Kimarekani 190,000; na

h) Gharama za usimamizi wa UNEP, wahandisi, waratibu na kununua vitendea kazi: Dola za Kimarekani 757,064

### 4.1.2 mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi maeneo ya bagamoyo, pangani, rufiji na zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Mwanzoni mwa mwaka 2009 Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*The Global Environmental Facility – GEF*), wenye makao makuu Washington, Marekani ulikubali mradi uliotajwa hapo juu. Mchakato ulichukua muda kidogo lakini Desemba mwaka 2011 GEF ikaridhia kutoa Dola Milioni tatu

na laki tatu (USD 3.36 million) kuisaidia Tanzania kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Bagamoyo, Rufiji, Pangani na Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la mradi huu lilikuwa ni Kujenga Ukuta wa Pangani uliokuwa umeharibiwa na kuongezeka kwa bahari. Mradi ulipaswa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano yaani kuanzia tarehe 30 Aprili 2012 hadi 31 Machi 2017 na fedha zilishatolewa na Utekelezaji wa mradi ulikuwa tayari umeshaanza. Maeneo ya mradi ni Pangani mjini; Bagamoyo (vijiji vya Kaole, Kwamduma, Kibindu, Kwamsanja, Saadani na Makaruge); Rufiji (Nyamisati Delta); Zanzibar: Pemba (Tumbe East na West, Ukele, na Kisiwa Panza) na Unguja (eneo la Bwawani).

**Mheshimiwa Spika,** Ufadhili wa mradi huu ulipitia dirisha la Mfuko wa Nchi Maskini Duniani ( *The Least Developed Countries Fund – LDCF*) ambao ulianzishwa mwaka 2001 (LDCs) zilizowanachama wa mkataba wa mabailiko ya tabinachi. Ni mwendelezo wa msaada kutoka mfuko huu ambapo mwaka 2007 Tanzania ilisaidiwa kuandaa mpango wa haraka wa Taifa wa kukabiliana na athari za mabailiko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulikuwa ufanye mambo yafuatayo ;

a) Kukarabati na kuimarisha ukuta wa Bahari ulioharibika maingilio ya mto Pangani katika bahari ya hindi (urefu usiopungua nusu kilomita kwa pande zote mbili za mto) na kupanda mikoko upya kupunguza kasi ya mawimbi katika baadhi ya maeneo ya ukuta, Dola za Kimarekani 1,100,000

b) Kuhamisha visima 18 vilivyoingiliwa na maji ya chumvi katika Wilaya ya Bagamoyo na kujenga vipya; Dola za Kimarekani 450,000

c) Kuhifadhi mikoko (3,000ha) katika mwambao wa Pwani ya Bahari ya Hindi katika wilaya ya Rufiji hasa maeneo ya nyamisati, Dola za Kimarekani 550,000

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Zanzibar zilitengwa kiasi cha Dola za Kimarekani 361,300 kwa ajili ya kazi zifuatazo;

a) Uhifadhi wa mikoko 50ha katika maeneo ya Tumbe na 100ha katika maeneo ya Ukele, Zanzibar;

d) Uimarishaji wa ukuta wa Bahari maeneo ya Bwawani hotel (urefu 120m), kupanda 50ha za mikoko, na kulinda maeneo ya ukanda wa Bahari Pemba (400m maeneo ya Ukele);

e) Uimarishaji wa ukuta wa Bahari maeneo ya Kisiwa Panza (urefu 50m na kuhimarisha 260ha za mikoko);

f) Kukuza uelewa wa mabadiliko ya tabianchi;

g) Kutathmini madhara ya mabadiliko ya tabianchi katika jamii.

Aidha zilitolewa fedha kwa ajili ya kazi zifuatazo;

a) Kuandaa na kusambaza masuala mbalimbali ya kisera: Dola za Kimarekani 225,000

b) Kujenga uelewa wa kuhusu mabadiliko ya tabianchi: Dola za Kimarekani 345,000

c) Gharama za usimamizi wa utekelezaji wa mradi na kununua vitendea kazi: Dola za Kimarekani 325,000

**Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya upinzani Bungeni imeshangazwa sana na kitendo cha serikali hii ya CCM kuomba fedha kwenye Mwaka huu wa fedha 2016/2017 kiasi cha shilingi bilioni 9.247 (kifungu 5001-idara ya mazingira) kwa ajili ya kufanya kazi ileile ambayo ilishatengewa fedha na wafadhili na zilishatolewa kama nilivyoainisha hapo awali.**

**Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni** ina taarifa za kina kuwa miradi hii miwili ilikumbwa na ufisadi mkubwa ambao ulikuwa ukiendeshwa baina ya Mtumishi Mmoja aliyeko katika Ofisi ya Makamu wa Rais idara ya mabadiliko ya tabia nchi akishirikiana na kigogo mmoja

aliyekuwa Ikulu wakati wa utawala wa awamu ya nne katika kutafuna fedha ambazo zilikuwa zimetolewa na wafadhili.

**Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni,** inaitaka Ofisi ya Makamu wa Rais imtake Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanyie ukaguzi maalumu (**Special Audit**) wa miradi hii miwili ya kupambana na mabadiliko ya Tabia nchi , pamoja na miradi mingine yote iliyosimamiwa na kitengo cha Mabadiliko ya tabianchi kilichopo chini ya Idara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais ,Mazingira na Muungano ,kwani kuna majipu ya kutumbua !.

Aidha tunalishauri Bunge lisitishe kupitisha maombi ya fedha ya mradi huu **kifungu 5001-idara ya mazingira** hadi hapo ukaguzi maalum utakapofanyika kuhusu fedha za mradi huu ambazo zilikuwa zimetolewa na wafadhili tajwa hapo juu utakapokamilika.

### 4.1.3 mabadiliko ya tabia nchi na hatari ya visiwa vyetu kutoweka

**Mheshimiwa Spika,** Hapo kale, kulikuwa na Kisiwa Miaka mingi iliyopita, mababu na mabibi zetu walipokuwa vijana kulikuwa na kisiwa baina ya Pemba na bara kilichoitwa **Maziwe**. Maziwe ilikuwa imefunikwa na mikoko iliyomea sana pamoja na msitu wa mwambao, na ilizungukwa na

mwamba mzuri wa matumbawe (coral reefs) na kujaa samaki. Kisiwa kilikuwa maarufu kwa upatikananji wa kasa. Mamia ya aina kasa kijana na kasa wa kawaida walikuja kutaga katika fukwe zenye mchanga za Maziwe kila mwaka. Kilikuwa kisiwa kizuri sana na kilichojaa wanyama pori hata kufikia kuteuliwa kuwa eneo la hifadhi ya marina mnamo mwaka 1975.

**Mheshimiwa Spika,** Hakukuwa na watu walioishi huo muda wote, japo kuwa lilikuwa eneo la hifadhi. Lilitumiwa na wavuvi wengi kama kambi. Walikusanya kuni kutoka msituni kupikia chakula chao, na kujenga vibanda kwa kutumia miti ya mikoko na makuti ya mnazi. Jambo hili liliendelea kwa siku nyingi. Lakini pole pole, bila ya mtu yoyote kujua msitu huo ulikuwa unatoweka. Mwanzo kulikuwa na wavuvi wachache lakini baada ya karne nyingi wavuvi wengi zaidi walikuja na kila walipokuja, kila mtu alikata au kuchoma matawi na miti machache tu. Lakini siku baada ya siku, mwaka baada ya mwaka, jambo hili liliongezeka na ilipofikia katika miaka ya sabini hakukuwa na mti hata mmoja kisiwani hapo. Maziwe ilikuwa sio chochote isipokuwa mchanga mtupu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa miaka michache baadaye, wavuvi waliendelea kukitumia kisiwa cha Maziwe, lakini hawakuweza tena kuoka moto na hakukuwa na kinga yoyote kutokana na

hali hewa inayobadilika au hali ya hewa mbaya. Mnamo mwaka 1978, janga lilitokea. Wakati wa upepo wa msimu dhoruba kali ililipiga kisiwani hapo. Kwa kuwa hakikuwa na miti ya kukihifadhi, mawimbi, makali yaliondosha kabisa sehemu ya juu ya kisiwa hicho na kuupeleka mchanga wote baharini, na kwenye miyamba ya matumbawe. Sasa kinachoweza kuonekana juu ya kisiwa hicho ni ukingo wa mchanga ambao unaweza kuonekana tu nyakati za maji kame, kasa hawana tena mahali pa kutaga mayai yao na hakuna kitu chochote kilichobaki kwa ajili ya watu. Kisiwa chote cha Maziwe kimeondolewa/kimetoweka .

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya kutoweka kwa kisiwa hiki cha **Maziwe** inapaswa kutukumbusha na kutufundisha jambo moja kuwa kuna hatari ya visiwa vyetu vingi kutoweka kama hatutachukua hatua za haraka za kuhifadhi visiwa vyetu.
Tunapata taarifa za hali ilivyo katika baadhi ya visiwa vya Pemba na Unguja kuwa katika tishio la kutoweka na taarifa mbalimbali za kisayansi zinaonyesha na kuthibitisha hivyo.
**Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni** inataka kujua ni hatua gani mahususi zinachukuliwa na serikali katika kukabiliana na hali hii ya tishio la kutoweka kwa baadhi ya visiwa vyetu Nchini?

## 5.0 MRADI WA DART NA UHARIBIFU WA MAZINGIRA BONDE - JANGWANI.

**Mheshimiwa Spika**, tabia ya serikali ya kufanya kazi bila kuwashirikisha wataalamu wa mazingira na wadau muhimu katika shughuli za mazingira kuanzia kwenye mipango yake mara nyingi umekuwa ukiigharimu sana serikali. Mathalani, Mradi wa mabasi yaendayo kasi Jijini Dar es Salaam unaojulikana kama **"DART PROJECT"**ambao umekuwa sehemu ya kuharibu mazingira kwa kuwa haukuzingatia taratibu za utunzaji wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa DART ambao umepita eneo la Bonde la Mto Msimbazi  kituo cha mabasi cha Jangwani umekuwa sehemu kubwa ya uharibifu wa mazingira kwa kuwa umezuia kingo za mto(river bank) katika eneo hilo la Jangwani na kusababisha mafuriko makubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ambao uliidhinishwa kwa mujibu wa kifungu cha (57) cha Sheria za Mazingira ya mwaka 2004 inasema kuwa "*(1) Kwa kuzingatia kifungu cha (2), ndani ya mita sitini hakutafanyika shughuli yoyote ya binadamu ya kudumu au ambayo kwa asili yake inaweza kuhatarisha au kuathiri vibaya ulinzi wa mazingira na, au utunzaji wa bahari au kingo za mto, bwawa, au miambao ya asili ya ziwa. (2) Waziri anaweza kuweka miongozo ya kuendesha shughuli za binadamu ndani ya maeneo yaliyoelezwa kwa mujibu wa kifungu cha (1)*. Mradi huu pia

ulipata Baraka za Baraza la Mazingira la Taifa, (National Environmental Management Council -NEMC).

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba mradi huu umeidhinishwa na Waziri anayeshughulikia mazingira haukufanyiwa tathimini ya muda mrefu ya kuzuia uharibufu wa mazingira (environmental mitigation measures). Maji yanayopita katika bonde hilo yamepoteza uelekeo wake wa asili na hivyo kutiririka mpaka kwenye maeneo ya makazi. Eneo hilo limegeuka kuwa sehemu ya kutuama maji (water retention area) na hivyo kuwa hatari sana kwani linaweza kuwa chanzo cha magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni moja tu kati ya miradi mingi inayofanywa na serikali bila kuzingatia athari za muda mrefu(long term impact) kama ulivyo kwa mradi wa DART kwenye suala la mazingira. Miradi ya namna hii imekuwa ikiiletea hasara serikali kutokana na athari zinazotokana na maamuzi yasiyozingatia utaalamu na ushauri kutoka maeneo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kueleza mbele ya Bunge lako ni hatua gani za dharura zitachukuliwa kuzuia athari za kimazingira zinazohatarisha maisha ya wakazi wanaoishi karibu na maeneo hayo? Serikali ieleze mbele ya bunge lako ni hatua gani stahili

zitakachukuliwa dhidi ya wale walioishauri serikali katika mradi huu bila kufanya tathimini maana?

## 6.0 UTAFUTAJI WA GESI ASILIA NA MAFUTA-NA HATIMA YA MAZINGIRA YETU

**Mheshimiwa Spika**, Inaeleweka kuwa Tanzania ni nchi ambayo inaelekea kwenye uchumi wa gesi na mafuta. Kama hivyo ndivyo, kwa vyovyote vile suala la utunzaji wa mazingira ni muhimu likawa kipaumbele kwa nchi ambayo inaendelea kama ya kwetu.

**Mheshimiwa Spika**, Baraza la Mazingira la Taifa ndilo lenye mamlaka ya kisheria na kikanuni ya utunzaji wa mazingira na kuhakikisha kuwa kunakuwa na matumizi endelevu ya rasilimali zetu kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, suala la utafutaji, uzalishaji, usafirishaji na hatimaye uuzaji wa gesi na mafuta usipoangaliwa ipasavyo unaweza kuwa janga kubwa la kimazingira katika bahari na hata katika maeneo ya nchi kavu.

**Mheshimiwa Spika**, athari za mazingira zitokanazo na masuala ya gesi na mafuta zinaenda mbali kuathiri maisha ya watu wanaishi karibu na miradi hiyo pamoja na viumbe

waliopo baharini kwa ujumla na hivyo kuathiri moja kwa moja uchumi wa maeneo husika kutokana na mabadiliko ambayo huletwa na shughuli hizo kama vile ukosefu wa ardhi yenye rutuba ambayo ingeweza kutumika kwenye kilimo pamoja uchafuzi wa vyanzo vya maji.

**Mheshimiwa Spika,** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa fedha za serikali katika taarifa yake ya mwezi Machi 2016 kuhusu taarifa ya ukaguzi wa ufanisi kuhusu masuala ya Sera ya Mazingira, Sheria na Kanuni za mazingira katika utafutaji wa mafuta imeonesha ni jinsi gani kama taifa hatujajipanga katika kuhakikisha kuwa mazingira yetu yanatunzwa katika michakato yote ya mafuta na gesi katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa fedha za serikali imegundua masuala muhimu ya kimazingira katika utafutaji wa mafuta na gesi kama ifuatavyo;

(i) Baraza la Mazingira la Taifa (NEMC)halina mpango mahususi wa kufanya ukaguzi katika miradi ya utafutaji mafuta na gesi kutokana na kutokuwa na vifaa, sekta hiyo ni mpya na pia Makampuni yanayoshughulika na sekta hiyo hutumia teknolojia ya hali ya juu sana.

(ii) NEMC haina Kanzidata ya makampuni yanayoshughulika na utafutaji wa mafuta na gesi

zaidi ya yale machache ambayo yamepewa vyeti vya tathmini ya mazingira.

(iii) Kwa miaka mitano mfululizo kati ya Makampuni 71 ya utafutaji gesi na mafuta NEMC wamefanikiwa kufanya ukaguzi kwenye makampuni matatu tu.

(iv) NEMC haina taarifa zinazojitosheleza za ukaguzi wa makampuni yanayoshughulika na utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi.

(v) Makampuni ya utafutaji wa mafuta na gesi yalishindwa kuwasilisha taarifa za mwaka za uzingatiwaji wa taratibu wa mazingira, pamoja na NEMC kueleza kuwa taarifa za makampuni zilipokelewa lakini hawakuweza kuwasilisha vielelezo kwa Mkaguzi na Mdhibiti wa Fedha za serikali.

(vi) Hakuna uratibu wa kiserikali wa kushughulikia masuala ya mazingira katika makampuni ya utafutaji wa mafuta na gesi, mathalani NEMC na Wizara ya Nishati na Madini hawashirikiani katika masuala ya mazingira katika sekta hiyo ikitiliwa mkazo kuwa TPDC ina kitengo cha mazingira ambacho kina taarifa za kina lakini hazipelekwi wala kuratibiwa kwa kushirikiana na NEMC.

(vii) Udhaifu wa kufuatili adhabu zinazotolewa dhidi ya makampuni yanayokiuka masharti ya utanzaji wa mazingira. Mathalani iligundulika kuwa Halmashauri

ya Mtwara ilitoa adhabu kwa kampuni ya gesi iliyokuwa imechafua maji ambayo ilikuwa inatumia na watu katika maeneo hayo lakini NEMC haikuweza kufuatilia utekelezaji wa adhabu hiyo.

(viii) Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira haina mkakati na wala usimamizi wa karibu wa NEMC pamoja na kuwa kisheria na kimsingi ofisi hiyo ndiyo inayosimamia Baraza hilo. Hata hivyo sababu iliyotolewa ni kuwa hakuna utaratibu mahususi uliotolewa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** serikali hii imekuwa na tabia ya kupuuzia masuala mbalimbali yanayoshauriwa na Mdhibiti na Mkaguzi wa fedha za serikali na pia ushauri wa bure unaotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kupuuza huko tusishangae nchi yetu hasa maeneo ambapo uchimbaji wa gesi na mafuta unafanyika yakatokea majanga makubwa ya kimazingira kama yaliyowahi kutokea huko Nigera na Mexico. **Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni** inaitaka serikali kuja na mkakati na mpango mahususi ambao utahakikisha mazingira yetu na watu wake yanakuwa salama na endelevu wakati wa zoezi la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa na kituko katika serikali hii kuwa kwa miaka

mingi serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira pamoja na kuwa na jukumu la moja kwa moja kusimamia NEMC bado hakuna hata utaratibu wa kutekeleza jukumu hilo na kwa maana hiyo Baraza hilo linajitegemea katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, sasa ni wakati mwafaka kwa serikali kupitia ofisi ya Makamu wa Rais kuhakikisha kuwa inasimamia mazingira katika miradi ya gesi na mafuta kwa mujibu wa sheria na kuacha visingizio vya miaka mingi ili kuelewa masuala mbalimbali ambayo yanaendelea katika miradi hiyo. Ni aibu kubwa kwa serikali ambayo kwa miaka mitano kati ya miradi ya gesi na mafuta 71 iliyokaguliwa ni miradi matatu pekee.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA 2015/16 NA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2015/16 Bunge liliidhinishia jumla ya shilingi 35,335,754,000/- kati ya fedha hizo shilingi 3,868,847,000/- ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Lakini hadi kufikia tarehe 31 march fedha za maendeleo zilipokelewa ni jumla ya shilingi 338,079,000/- tu ambayo ni sawa na asilimia 8.7 ya fedha zote za maendeleo zilizopitishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Rais inaomba jumla ya shilingi 17,627,025,000/- kwa mwaka wa fedha 2016/17 ili kutekeleza majuku yake zikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 10,747,250,000/- zimetengwa kama fedha za maendeleo, na kati ya hizo shilingi 8,000,000,000/- ni fedha za ndani na shilingi 2,747,250,000/- ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Ukiangalia ni kwamba bajeti ya mwaka huu ni nunu ya bajeti ya mwaka jana, japokuwa bajeti ya fedha za maendeleo kwa mwaka huu ni takriban mara tatu ya bajeti iliyotengwa mwaka jana. Kama bajeti ya mwaka jana ilitolewa asilimia 8.7. Hoja ni je hizi za mwaka huu zitaweza kutekelezwa hata kwa nusu? Kwanini tusipange kulingana na kile tulichonacho? Badala ya kuonesha kuwa bajeti ni kubwa kwenye makaratasi tu. Lakini hali halisi ni kuwa hela hakuna.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa kamanchi tunatakiwa kuwa na sera inayojitegemea inayohusu Mabadiliko ya Tabianchi, kwani madhara yake ni dhahiri yataonekana kama bado lakini yatakuja na fedha zinazopatika kutoka kwa wadau badala ya kutumiwa kwa lengo hilo zinaingia kwenye mifuko binafsi. Wahusika ni sawa au zaidi ya wahujumu wa uchumi kwa nchi yetu.

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia ushauri wetu ili nchi yetu iwe ni eneo salama la kuishi kwa vizazi vyetu.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani,

Naomba kuwasilisha,

**…………………………………..**

**Pauline P. Gekul (Mb)**

**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira.**

**02.05.2016**